# *BARUA #03; MAANA YA UHURU KAMILI NA JINSI YA KUUFIKIA.*

Kwako rafiki yangu mpendwa,

Moja ya hitaji kubwa kwenye maisha yako ni kufikia UHURU KAMILI wa maisha yako.

Uweze kuyaishi maisha yako kwa namna unavyotaka wewe mwenyewe bila ya kulazimika kufanya usichotaka kufanya.

Lakini je uhuru kamili ni nini hasa? Na unawezaje kufikia uhuru huo?

Haya ni maswali ambayo wengi huwa hawayajibu mapema na hivyo kujikuta wamejiingiza kwenye mambo ambayo yanawazuia wasiwe huru.

Kwenye barua ya leo, tunakwenda kujifunza kwa kina kuhusu uhuru kamili na jinsi ya kuufikia.

Uhuru ni moja ya mahitaji makubwa mawili ya maisha ambayo kila mmoja wetu anapigania, hitaji kuu la pili ni furaha, ambalo tutaliangalia kwenye barua itakayofuata.

Barua ya leo tutaangalia kwa kina kuhusu uhuru kamili.

Tukianza na maana ya uhuru, ni pale unapoishi vile unavyotaka wewe, pale unapofanya maamuzi kulingana na mahitaji yako na hulazimiki kufanya usichotaka ili kuwaridhisha au kuwafurahisha wengine.

Pamoja na kwamba uhuru unajiangalia wewe, lakini kila uhuru huwa una mipaka yake. Uhuru bila mipaka unageuka kuwa ukatili. Kwa sababu kwenye maisha kama kila kitu utajiangalia mwenyewe tu, kuna wengine wataumia.

Ndiyo maana kwenye KISIMA CHA MAARIFA, imani yetu kuu ni kwenye UPENDO, ambao unaanza na kujipenda sisi wenyewe, kuwapenda wengine na kupenda kile tunachofanya.

Iwapo utaongozwa na upendo, unapochagua kuyaishi maisha yako vile unavyotaka wewe, hutajiumiza wewe wala kuwaumiza wengine. Hutafanya kitu cha kukudhuru wewe au kuwadhuru wengine.

Ndiyo unataka kuwa huru utakavyo, lakini haimaanishi kujidhuru wewe na kuwadhuru wengine.

Wengi wanaokosa msingi sahihi wa upendo, wanapotafuta na kutumia uhuru wao, huishia kuleta maumivu kwao na kwa wengine.

Ukiangalia historia ya dunia, watu wote ambao walikuja kugeuka na kuwa makatili na wauaji wakubwa, walianza kwa nia njema kabisa ya kutaka kuwasaidia watu, lakini kwa kukosa misingi sahihi walijikuta wakileta madhara makubwa kwao na kwa wengine.

Hili ni jambo la kuchunga na kuwa nalo makini mno kwenye safari yetu ya mafanikio, msingi mkuu wa kwanza na muhimu ni UPENDO, kwetu wenyewe, kwa wengine na kwa kile tunachofanya.

Bila ya upendo, uhuru unageuka kuwa ukatili ambao haumuachi mtu yeyote salama, hata yule ambaye anao.

Kitu muhimu sana cha kujua na kuzingatia kwenye uhuru ni kwamba hakuna yeyote atakayekupa uhuru. Ni kitu ambacho unapaswa kukifanyia kazi mwenyewe, kwa kuanzia ndani yako ili uweze kukifikia.

Unapaswa kujua pia kwamba nguvu mbalimbali zitakuwa zinakuzuia usiwe huru, hivyo unapaswa kuzijua na jinsi ya kukabiliana nazo kama kweli unataka kufikia uhuru kamili wa maisha yako.

Kwenye barua hii, tutakwenda kujadili aina tano za uhuru na jinsi ya kuweza kuzifikia kwenye maisha yetu.

## UHURU BINAFSI.

Uhuru binafsi ni kuwa huru kuishi vile unavyochagua wewe. Hii ni sehemu ya kwanza na muhimu kabisa ya uhuru ambayo wengi huwa hawaizingatii.

Kuna mahitaji makubwa matatu ya kukuwezesha kufikia uhuru binafsi.

## Kujitambua.

Hitaji la kwanza la uhuru binafsi ni kujitambua wewe mwenyewe, huu ndiyo msingi mkuu wa falsafa zote, 'know thyself'.

Bila ya kujitambua wewe mwenyewe, huwezi kuwa na uhuru binafsi, kwa sababu hutajua nini unataka na nini hutaki, badala yake utaishia kuiga kile ambacho wengine wanafanya.

Mpaka sasa nina imani kubwa umeshajitambua wewe mwenyewe, unalijua kusudi la maisha yako hapa duniani, unajua nini unapenda na nini hupendi, unajua uimara wako na udhaifu wako uko wapi.

Kwa kujijua hivi, unachagua maisha yanayoendana na wewe, hujilinganishi wala kushindana na wengine kwa sababu unajua wao siyo wewe, hakuna yeyote aliye kama wewe hivyo kujilinganisha au kushindana na wengine ni kujipoteza mwenyewe.

## Unyenyekevu.

Hitaji la pili kwenye uhuru binafsi ni unyenyekevu, bila ya unyenyekevu huwezi kufikia uhuru binafsi na hata ukiufikia hautakuwa na manufaa kwa yeyote na hautadumu.

Unyenyekevu ni kutambua kwamba siyo kila kitu kitakuja kwako kwa wakati ambao unataka. Hata uwe nani, huna nguvu ya kupata kila unachotaka kwa wakati unaotaka. Wewe unapanga utakavyo lakini dunia inaenda inavyokwenda, haikuangalii wewe.

Unyenyekevu ni kupokea matokeo unayoyapata na kisha kuyatumia kwa namna ambayo ni bora zaidi. Siyo kulalamika kwa sababu hujapata unachotaka au kukata tamaa kwa sababu matokeo yamekuja tofauti na ulivyopanga.

Unapopanga ni kama unajipa mwongozo wa hatua zipi uchukue, hivyo udhibiti wako upo kwenye hatua unazochukua pekee. Matokeo utakayoyapata yako nje kabisa ya uwezo wako. Kadiri unavyochukua hatua utakutana na bahati

na hatari ambazo usingeweza kuziona kabla na kuzipangilia.

Ndiyo maana ni muhimu sana ukishaweka mpango na kuufanyia kazi, kwa kila matokeo unayoyapata kuboresha zaidi mpango wako.

Unyenyekevu unakusaidia kuamini kwenye mchakato, ukijua kwa kuwa unafanya kilicho sahihi, basi ni swala la muda tu kupata matokeo ambayo ni sahihi.

Kwa sababu unataka kuwa na uhuru kamili, haimaanishi kila kitu kitakwenda kama utakavyo wewe, kuwa mnyenyekevu, kuwa na subira na mara zote chukua hatua sahihi bila kulalamika au kukata tamaa.

## Kuwa tayari kupoteza kila kitu.

Hitaji la tatu kwenye uhuru binafsi ni kujua huhitaji chochote. Hili linaweza kukuchanganya kidogo, kwamba uhuru unamaanisha kuishi utakavyo na kupata unachotaka, lakini pia uhuru unakutana usihitaji chochote, imekaaje hiyo?

Iko hivi rafiki, chochote kile ulichonacho kwenye maisha yako, utakipoteza, huo ni uhakika, ni adhabu uliyopewa siku ambayo ulizaliwa. Hata maisha uliyonayo tu utayapoteza, kwa sababu kuna siku utakufa.

Kila ulichopambana na kuwa nacho kwenye maisha, kuna siku utakipoteza. Hivyo uhuru kamili kwenye maisha, ni kuwa tayari kupoteza kila kitu na bado maisha yako yasitetereke.

Kinachowanyima wengi uhuru kamili kwenye maisha ni kujishikiza kwenye kile walichonacho. Wanakuwa wamepambana sana kupata kitu au nafasi fulani na baada ya kufikia hali hiyo wanaishi maisha yao yote kwa hofu ya kupoteza kile walichopata. Na inapotokea wamepoteza basi maisha yao yanavurugika kabisa.

Usiruhusu hilo, pambana kupata chochote unachotaka, lakini kuwa tayari kwa wakati wowote kukipoteza na hapo usiruhusu maisha yako yakavurugika.

Kwa kujua kusudi laki na kwa kuwa na misingi unayoiishi, hivyo ndiyo muhimu, mengine

yanakuja na kuondoka, lakini wewe unabaki umesimama imara.

Wale wasiokuwa tayari kupoteza kile walichonacho ndiyo ambao hawana uhuru kabisa kwenye maisha yao.

Unakuta mtu amepambana kweli kujenga biashara au kazi yake, kwa kuishi misingi aliyoichagua ambayo ni sahihi kwake. Kisha anakuja kutokea mtu mwenye mamlaka fulani ambaye anamlazimisha afanye kitu ambacho siyo sahihi kwa kumtishia asipofanya ataharibu kile alichojenga.

Kwa akili za haraka mtu anaweza kujiambia ni bora nifanye ili nisipoteze nilichopambana kujenga, lakini akishakubali hivyo tu, basi anakuwa amepoteza uhuru wake wote, kwani atazidi kubanwa kwa namna hiyo kufanya yasiyo sahihi.

Watu wakishajua ni kitu gani haupo tayari kukipoteza, watakitumia hicho kukutawala na kukutumia watakavyo. Kama upo tayari kupoteza chochote kile na maisha yako

yasitetereke, unakuwa huru kabisa na hakuna anayeweza kukutishia chochote.

Uhuru binafsi ndiyo mahali pa kuanzia, KUJITAMBUA MWENYEWE, KUWA MNYENYEKEVU na KUWA TAYARI KUPOTEZA KILA KITU, haya matatu ni muhimu kwenye kujijengea uhuru binafsi.

## UHURU WA FEDHA.

Ukiondoa hewa tunayopumua, fedha ndiyo kitu cha pili kwa umuhimu kwenye maisha yetu. Na kuna wakati fedha inaweza kuwa kitu cha kwanza, hasa pale mtu anaposhindwa kuivuta hewa hiyo mwenyewe na kuhitaji msaada wa kitaalamu kumwezesha kuivuta.

Hivyo baada ya kupata uhuru binafsi, uhuru wa pili kujijengea ni uhuru wa kifedha.

Uhuru wa kifedha ni muhimu kwa sababu unakuwezesha kupata sehemu kubwa ya yale unayotaka. Lakini muhimu zaidi uhuru wa kifedha unakupa uhuru mwingine muhimu zaidi ambao ni UHURU WA MUDA.

Unapokuwa na uhuru wa kifedha unakuwa na uhuru na muda wako kwa kuweza kuutumia utakavyo. Lakini ukikosa uhuru wa kifedha, muda unakuwa siyo wako, yeyote anayekulipa ndiye atakayedhibiti muda wako, atakupangia wakati gani uamke, uwe wapi kwa wakati gani na wakati gani upumzike.

Vitu vingi unavyohitaji kwenye maisha yako unavipata kupitia fedha. Na hata kuendesha maisha yako kwa kawaida, unahitaji fedha. Hivyo fedha ni muhimu na usiibeze kwa namna yoyote ile.

**Kwenye uhuru wa fedha, kuna mambo matano muhimu ya kuzingatia.**

## Matumizi yasizidi kipato.

Jambo la kwanza na muhimu ni matumizi kutokuzidi kipato. Unataka kuwa huru, unataka kupata kila unachotaka kwa namna unavyotaka wewe. Lakini kama unachotaka kiko juu ya uwezo wako, unachotafuta siyo uhuru, bali utumwa.

Utumwa wa kwanza ambao watu wamekuwa wanautengeneza kwenye maisha ni kupitia kukopa, hasa vitu ambavyo havizalishi. Unapokopa ili kuendesha maisha yako ya kawaida, hutengenezi uhuru, unatengeneza utumwa. Anayekudai anakudhibiti, anakunyima uhuru, na ubaya ni umepoteza uhuru wako kwa vitu ambavyo huwezi hata kuviona.

Hivyo hatua ya kwanza kabisa, bila ya kujali kipato chako ni kidogo au kikubwa kiasi gani, matumizi yako hayapaswi kuzidi kipato chako. Kuishi chini ya kipato chako siyo utumwa, bali ni kujenga uhuru. Kuacha kununua kile unachotaka kwa sababu huna fedha wakati huo siyo utumwa, bali ni uhuru kwa sababu unaepuka kujiingiza kwenye deni ambalo litakutesa zaidi.

Jua kipato chako na ishi chini ya kipato chako, usijikweze, usiishi maisha ya kuonekana ambayo yatakuweka kwenye utumwa wa madeni.

Epuka mno madeni kwenye maisha yako, kamwe usikope fedha kwa matumizi ya maisha kama chakula, mavazi, pango, ujenzi, usafiri na matumizi mengine yoyote ambayo hayazalishi faida.

Kama kipato chako ni kidogo, shusha maisha yako chini ya kipato hicho na kazana kukikuza kipato chako. Na siyo kuishi juu ya kipato chako kwa madeni ambayo yatakunyima uhuru zaidi.

Kingine muhimu sana cha kujua hapa ni kwamba matumizi huwa yanakua kadiri kipato kinavyoongezeka, hivyo kama hutakuwa na udhibiti, hata ukiongeza kipato kiasi gani, bado hakiwezi kutosha.

## Akiba ya kuendesha maisha bila kipato.

Jambo la pili ni kuwa na akiba ya kuweza kuendesha maisha yako. Hili ni eneo muhimu la uhuru wa kifedha ambalo wengi huwa hawalipi uzito. Watu wengi wamekosa uhuru kwenye maisha kwa sababu wanaishi maisha ya mkono kwenda kinywani.

Yaani ana kipato kizuri, lakini akishakipata anakitumia chote na kusubiri tena kipato kingine. Hivyo ikitokea changamoto yoyote kwenye kipato chake, anakuwa hana uwezo wa kuendesha maisha yake.

Mfano kama mtu amesimamishwa kazi ghafla, au biashara imeyumba, hana akiba ya kuweza kuyaendesha maisha yake wakati anasubiri mambo yakae sawa. Katika hali hiyo mtu anakuwa kwenye hali inayomsukuma kukubaliana na chochote ili tu apate chochote cha kuendesha maisha yake.

Kutegemea kipato kijacho ili kuendesha maisha yako ni utumwa mbaya mno unaojijengea. Na utumwa mbaya zaidi ni pale unapokopa kwa kipato ambacho bado hujawa nacho. Mfano leo ni tarehe 10, kuna uhitaji unao ila fedha huna, unajua mshahara utaingia tarehe 30, basi unakopa leo kwa kuahidi kulipa mshahara utakapotoka, ni utumwa mbaya mno.

Kuondokana na utumwa huu, katika wakati wowote ule, hakikisha una akiba ya

kukuwezesha kuendesha maisha yako kwa miezi 6 mpaka 12 ijayo hata kama hutaingiza kipato chochote kile katika kipindi hicho.

Yaani hata kama una uhakika mshahara utaendelea kuingia au biashara itaendelea kuzalisha faida, hakikisha una hiyo akiba ya fedha umeitunza. Uhakika wowote unaojipa unajidanganya, tumeshaona kwamba sisi tunapanga na dunia inafanya yake.

Sihitaji kukushawishi sana kwenye hili kwa sababu mwaka 2020 umekuwa ushahidi mzuri mno kwetu. Janga la Corona limetuonesha jinsi gani mambo yanaweza kubadilika haraka kuliko tunavyoweza kutabiri au kujiandaa. Hii siyo mwanzo wala mwisho, kuna mengi yatakuja huko mbele ambayo hukuyategemea.

Hivyo wakati wowote ule, kuwa na akiba ya kuweza kuendesha maisha yako, kwa miezi sita mpaka mwaka hata kama huna kipato kabisa. Kokotoa gharama zako za msingi za kuendesha maisha yako kwa mwezi, kisha zidisha kwa

miezi sita au 12 na kiasi hicho kuwa nacho kama akiba.

Kwa kuwa na akiba hii, unakuwa na utulivu mkubwa kwa sababu unakuwa huru. Jambo lolote litakalotokea na kuathiri kipato chako halitakupa taharuki, kwani utakuwa na kipindi kirefu cha kujipanga na kurudi kwenye kuzalisha kipato.

Kama huna akiba yoyote, likitokea lolote kwenye kipato chako, unakuwa huna namna, utalazimika kutegemea huruma ya wengine au hata kuingia kwenye madeni zaidi ambayo yanaendelea kukunyima uhuru.

## Uwekezaji.

Jambo la tatu ni kuwa na uwekezaji unaozalisha faida. Haijalishi kwa sasa unafanya kazi au biashara inayolipa kiasi gani, hutaweza kufanya hivyo milele. Kadiri muda unavyokwenda unachoka na nguvu kupungua, hivyo hutaweza kuendelea kufanya kama unavyofanya sasa.

Lakini mahitaji ya maisha hayatakoma, kadiri umri wako unavyokwenda ndiyo mahitaji yako

yanazidi kuwa makubwa na muhimu, lakini uwezo wako wa kuzalisha zaidi unapungua.

Hivyo hapo unahitaji kuwa na njia ya kuingiza kipato bila ya kufanya kazi moja kwa moja. Na hapo ndipo uwekezaji unapokuja.

Katika kujijengea uhuru wa kifedha, unapaswa kuwa na uwekezaji ambao unazalisha faida bila ya wewe kufanya kazi moja kwa moja.

Unapofanya uwekezaji, zingatia vitu vikubwa vitatu, ukuaji wa thamani, uzalishaji wa faida na urahisi wa kugeuza uwekezaji wako kuwa fedha.

Watu wamekuwa wanawekeza bila ya mpango, wanajikuta wana uwekezaji mkubwa, ila wanapokuwa na uhitaji wa fedha kwa haraka, hawawezi kugeuza uwekezaji wao kuwa fedha.

Chukua mfano mtu unakuwa na heka 100 za miti ambazo zina thamani kubwa, unapata shida au dharura ya haraka ambayo inakutaka uwe na fedha za kutatua. Kama huo ndiyo uwekezaji pekee ulionao, utakuwa na ugumu

wa kupata fedha kwa sababu siyo rahisi kuugeuza uwekezaji huo kuwa fedha. Inachukua muda mpaka uweze kuuza shamba au miti hiyo.

Hivyo unapowekeza, zingatia sana vigezo hivyo vitatu, uwekezaji uongezeke thamani kadiri muda unavyokwenda, uweze kuvuna faida ya mara kwa mara huku uwekezaji ukiendelea kuwepo na katika uwekezaji unaofanya, kuwe na ambao ni rahisi kugeuza kuwa fedha.

Kwa aina za uwekezaji na jinsi ya kuzifanya rejea kwenye kitabu cha ELIMU YA MSINGI YA BIASHARA.

Lakini muhimu sana, anza mapema, wekeza mara kwa mara na acha uwekezaji wako ukue bila ya kuuingilia.

Kwa kutaja kwa uchache, aina za uwekezaji ambazo unapaswa kuwa nazo;

Moja ni biashara inayoweza kujiendesha mwenyewe bila ya wewe kuwepo. Kwa biashara yoyote unayofanya sasa, ijengee

mfumo wa kuweza kujiendesha yenyewe bila ya uwepo wako na kuiwezesha iwe imara na idumu kwa miaka mingi. Kwa njia hii, hata utakapokuwa umepumzika, utaendelea kupata faida kutoka kwenye biashara huku ikiendelea kukua. Usikubali wewe kuwa ndiyo kila kitu kwenye biashara yako.

Mbili ni kuwekeza kwenye masoko ya mitaji ambapo uwekezaji unakua thamani na hata kuzalisha faida. Pia ni rahisi kugeuza uwekezaji huo kuwa fedha. Miliki fedha na wekeza kwenye vipande vya UTT, huo ni uwekezaji unaopaswa kuwa nao kwa mazingira yetu na ufanye mara kwa mara. Kila mwezi tenga kiasi utakachowekeza huko.

Tatu ni kwenye mali zisizohamishika, hapa ndipo yanakuja majengo, viwanja, mashamba, miti na kadhalika. Huu ni uwekezaji ambao unatunza thamani kwa muda mrefu na unaoweza kuutumia kama nyenzo ya kufanya vitu vingine, hivyo jenga uwekezaji huu pia.

Hakikisha una uwekezaji, huwezi kufika kwenye uhuru wa kifedha kama hujawekeza, haijalishi unalipwa kiasi gani au unatengeneza faida kubwa kiasi gani, kama hutengenezi njia ya kuweza kuingiza kipato bila kufanya kazi, utakuwa mtumwa maisha yako yote.

## Mifereji mingi ya kipato.

Jambo la nne ni kutotegemea chanzo kimoja cha kipato. Hili sitalijadili sana, utaenda kusoma kwa kina zaidi kwenye kitabu cha ELIMU YA MSINGI YA FEDHA.

Lakini hapa nisisitize tu, huwezi kuwa huru kifedha kama unategemea chanzo kimoja cha kipato. Hata kiwe kikubwa kiasi gani, ukishakuwa na chanzo kimoja, umechagua utumwa.

Kwa sababu utalazimika kukilinda chanzo hicho hata kama ni kwa kupoteza uhuru wako. Pia tatizo lolote likitokea, linakuweka kwenye matatizo makubwa.

Kuwa na vyanzo mbadala, angalau vinne vya kukuingizia kipato ili kutengeneza uhuru wako.

Chanzo kimoja kikia na shinda, vingine vinaendelea kuingia na maisha hayasimami.

Kadhalika kwenye uwekezaji, lazima ufanye kwa njia mbalimbali na siyo eneo moja pekee.

Hata kwenye biashara, usitegemee mteja mmoja au wakubwa wachache, kuwa na wateja wengi ili yeyote asikufanye kuwa mtumwa kwake.

## Jilinde.

Jambo la tano ni kuwa na njia mbadala ya kutunza na kupata fedha zako kwa namna ambayo utaweza kuwa salama.

Hii ni dhana ngumu na muhimu ambayo unapaswa kuifanyia kazi kwa umakini mkubwa mno.

Iko hivi rafiki, unaweza kuwa na fedha nyingi, lakini usiwe na uhuru au usiwe salama, hasa kwa mamlaka mbalimbali ambazo zina nguvu juu ya kila mtu, mfano serikali.

Mabadiliko ya sera mbalimbali za serikali au kubadilika kwa utawala, kunaweza kukuathiri

sana wewe na fedha zako. Hivyo unapaswa kuwa na mkakati ambao unakulinda wewe na kuhakikisha hukosi uhuru kabisa.

Serikali zote duniani huwa zina nguvu kubwa na huwa hazishindwi kufanya kitu chochote, hata kama siyo cha haki. Hivyo unaweza kuwa unafanya kila kitu kwa usahihi kabisa, unafuta kila sheria, lakini ikatokea siku ukajikuta kwenye mikono ya serikali kwa namna moja au nyingine.

Kitu cha kwanza ambacho serikali itafanya ikishakuweka kwenye mikono yake ni kuhakikisha inaondoa kila nguvu uliyonayo, na kitu cha kwanza huwa ni kuzuia fedha na mali zako zote.

Hilo linaweza kutokea hata kama huna kosa lolote lile, labda tu umeshukiwa au kuna mtu amefanya kitu kukukomoa.

Pamoja na kuwa tayari kupoteza kila kitu, lazima pia uwe na maandalizi pale hali kama hiyo inapoweza kutokea. Na hali ya aina hiyo inaweza kutokea kwa kila mtu.

Baadhi ya njia za kutumia kujilinda na hali kama hii ni hizi;

Hatua ya kwanza na rahisi kabisa ni kuhakikisha katika kila wakati unakuwa na kiasi cha fedha taslimu. Usiweke akiba yako yote ikakaa benki au kwenye mifumo ambayo inaweza kufungwa mara moja na ukajikuta huna hata senti moja. Kuwa na kiasi cha fedha ambazo ni taslimu kiasi kwamba zilizopo kwenye mifumo mingine zikifungwa, unaweza kuendelea kuendesha maisha yako.

Njia nyingine ni kuwa na mali ambazo huzimiliki kama mtu binafsi, badala yake unazimiliki kama kampuni. Hilo ni muhimu kwa sababu hata kama kampuni ni yako, bado siyo wewe. Hivyo mali zako binafsi zikizuiwa, kampuni haiwezi kuzuiliwa.

Njia nyingine ni kutunza sehemu ya utajiri wako nje ya fedha za kawaida. Kuna njia kama madini ya dhahabu na mengineyo. Lakini kwa sasa kuna teknolojia mpya imekuja ya Cryptocurrency. Hizi ni njia ambazo kila mmoja

wetu anapaswa kuendelea kujifunza na kuona njia ya kuzitumia. Muhimu ni kuhakikisha unakuwa na fedha zako kwenye mfumo ambao siyo rahisi kuzimwa haraka na ukakosa kila kitu.

Njia nyingine unayoweza kutumia ni kuwa na baadhi ya mali au fedha kwa majina ya watu wa karibu kwako.

Njia nyingine ni kuhifadhi fedha zako kwa sarafu tofauti na nje ya nchi, ipo mifumo salama ya kufanya hivyo.

Haya ni mambo unayopaswa kuyafanyia kazi kadiri utajiri wako unavyokua kwa sababu unavyokwenda juu ndivyo unawindwa na wengi. Unaweza usiwe na kosa lolote na bado ukapitishwa kwenye misukosuko mbalimbali. Kuwa tayari kupoteza kila kitu ni njia ya kwanza ya kukufanya uendelee kubaki huru na kuwa na njia mbadala ya kuhifadhi fedha na utajiri wako ambayo haiwezi kuzimwa haraka ni njia ya kuhakikisha maisha yako yanaendelea hata utakapokuwa unapitia misukosuko mbalimbali.

Hapa tumejifunza njia mbalimbali za kujijengea uhuru wa kifedha, zizingatie na kadiri unavyokua weka ulinzi zaidi. Pia rejea kwenye kitabu cha ELIMU YA MSINGI YA FEDHA kujifunza mengine kwa kina kama kulinda utajiri, kodi na kutoa kwa wengine, vitu ambavyo ni muhimu kwenye kukinga uhuru wako wa kifedha.

## UHURU WA KAZI.

Kazi yoyote unayoifanya, iwe umeajiriwa au kujiajiri, unahitaji kuwa na uhuru mkubwa. Uhuru ndiyo unaokuwezesha kufanya kazi bora na ambayo itakuwezesha kufikia mafanikio makubwa kwenye maisha yako.

Watu wengi wamekuwa wanafanya kazi ambazo haziwapi uhuru, kitu kinachoyafanya maisha yao yasiwe huru na bora.

Ili kuwa na uhuru wa kazi, zingatia mambo haya matatu;

## Penda unachofanya.

Kitu cha kwanza na cha muhimu katika kufikia uhuru wa kazi ni kupenda kazi unayoifanya. Iwe umeichagua au umeipata tu, iwe ni kazi ya ndoto yako au siyo, penda sana kazi unayoifanya.

Ukishakubali tu kufanya kazi yoyote ile, ifanye kwa moyo wako wote, weka kila ulichonacho kwenye kazi hiyo. Usiangalie sana unalipwa nini, wewe angalia zaidi unafanya nini, ni thamani gani unayoitoa kupitia kazi hiyo.

Kwa kupenda kazi yako na kujituma kwenye kuifanya, utazalisha thamani kubwa na utategemewa na wengi kupitia kazi hiyo.

Ukishajenga utegemezi wa wengine kupitia unachofanya, unakuwa huru zaidi kuliko wewe kuwa ndiyo tegemezi kwa wengine.

Kila unapoifanya kazi yako, jiambie ndani yako unaipenda, kila unapomhudumia mwingine kupitia kazi yako, jiambie unampenda ndiyo maana unamhudumia.

Bila hata ya kufanya chochote cha ziada, kitendo tu cha kuipenda kazi yako kutoka ndani ya moyo wako, kitamfanya kila mtu ajue kweli unapenda na atajisikia vizuri kufanya kazi na wewe.

## Bobea.

Kingine kinachowakwamisha wengi kwenye kazi ni kutokuweza kuifanya vizuri. Unapaswa kubobea hasa kwenye kazi yako, jua kwa kina kile unachofanya na ujue jinsi ya kukifanya kwa ubora wa hali ya juu kabisa.

Usifanye chochote kwa kubahatisha, jua nini unafanya na jiamini kwenye kukifanya. Wale unaofanya nao kazi au unaowapa huduma, wanajua kabisa kama unajua au unabahatisha.

Kama umechagua kufanya kazi, ijue kwa undani, bobea.

Uzuri ni kwamba kwa zama tunazoishi sasa, fursa za kujifunza na kujua kwa kina kile unachofanya ni nyingi mno. Kupitia mtandao wa intaneti na vitabu kuna mafunzo mengi kuhusu kazi yoyote ile unayofanya.

Tenga angalau saa moja kila siku kujifunza zaidi kuhusu kazi unayoifanya. Kwa kufanya hivyo, kadiri unavyokwenda utakuwa na ubobezi mkubwa.

Kila siku tathmini kazi yako ilivyokwenda, changamoto ulizokutana nazo na yale uliyojifunza. Kila changamoto uliyoikabili, jifunze zaidi jinsi ya kuizuia isitokee au kukabiliana nayo kama itatokea tena.

Watu wengi sana wanafanya kazi zao kwa mazoea, wakishatoka shule hawajifunzi tena kuhusu kazi zao, mpaka labda wapelekwe kwenye mafunzo ya lazima au warudi tena kusoma.

Wewe ukichagua kubobea kwa kuwa na mfumo endelevu wa kujifunza, utafanya kazi yako kwa ubora kuliko wengine, hilo litafanya wewe utegemewe zaidi kitu ambacho kitakupa uhuru kwenye kazi unayoifanya.

## Jitofautishe.

Kama kuwepo au kutokuwepo kwako kwenye kazi hakuna tofauti, hauwezi kuwa huru kwenye

kazi hiyo. Kwa kifupi wewe ni mzigo ambao nafasi ya kupunguza mizigo ikitokea basi wewe ni wa kwanza kuondolewa.

Ninachosema ni kwamba kama umeajiriwa kwenye kazi na usipokuwepo hakuna chochote kinachokosekana, hiyo kazi unayo kwa sababu tu kufukuzwa ni mchakato mrefu. Ikitokea hali kwamba inabidi watu wapunguzwe, utakuwa mmoja wa wanaopunguzwa kwa sababu huna cha tofauti ambacho kinategemea.

Sehemu yoyote unayofanya kazi, hakikisha kuna kitu cha tofauti unachofanya ambacho kinategemewa sana na hakuna mtu mwingine yeyote anayeweza kukifanya ila wewe. Hata kama wengine watafundishwa, bado hakuna anayeweza kufanya kama wewe.

Ukiweza kufikia hili, unakuwa na uhuru mkubwa kwenye kazi hiyo, kwa sababu kuna kitu unashikilia. Unakuwa na nguvu ya kuweza kudai maslahi zaidi, unakuwa na nguvu ya kuweza kukataa yasiyo sahihi na huwi tu mtu wa kuvurugwa.

Hapa kuna ombwe kubwa mno, watu wengi wanafanya kazi zao kwa mazoea na kwa kusubiri kusukumwa. Kiasi kwamba kama wewe utachagua tu kufanya vitu vichache kwa utofauti, utajitofautisha mno na hao wengine na utakuwa unategemea na hilo litakuweka huru.

Ukianza kwa kupenda sana kile unachofanya na kisha kukazana kubobea kwenye kazi yako huku ukiwa na kitu cha tofauti ambacho hakuna mwingine anayeweza kukifanya, utakuwa huru kwenye kazi yako.

Unaijua kazi yako, unayajua mazingira yako ya kazi na unawajua wale unaofanya nao kazi na wanaotegemea kile unachofanya. Kaa chini kuyatafakari hayo kwa kina na chagua ni kwa namna gani utajitofautisha kabisa ili uwe wa kutegemewa kwenye kazi hiyo na ujijengee uhuru zaidi.

## UHURU WA BIASHARA.

Watu wanapokuwa wameajiriwa huwa wanaona hawapo huru, hivyo hutamani sana

kwenda kujiajiri au kuanzisha biashara zao wenyewe wakiamini ndiyo watakuwa huru.

Lakini wanapokwenda kufanya hivyo, wanagundua hawapo huru. Kwa sababu wengi wanaishia kuanzisha biashara ambazo zinawategemea wao kwa kila kitu. Hivyo hata kama ataifanya vizuri na ikaingiza faida, bado hana uhuru, kwa sababu asipokuwepo biashara haiwezi kujiendesha.

Katika kujijengea uhuru wa kibiashara, kuna mambo matatu ya kuzingatia.

## Mfumo.

Biashara yoyote ile unayoifanya, ijengee mfumo ambao utaiwezesha kujiendesha yenyewe hata kama wewe haupo.

Hakuna ubishi kwamba miaka ya mwanzo ya biashara itakutegemea zaidi wewe, lakini kadiri inavyokua jenga mfumo wa kuiwezesha ijiendeshe yenyewe.

Biashara iweze kwenda vizuri iwe upo au haupo.

Kujifunza jinsi ya kujenga mfumo wa kuendesha biashara yako, rejea mafunzo ya MFUMO WA BIASHARA ambayo yanapatikana kwenye KISIMA CHA MAARIFA. Unaweza kufungua hapa kuyapata;

## Kujitofautisha.

Kama ilivyo kwenye kazi, kama hakuna kinachowafanya wateja waache kwenda kwa wengine na kuja kwako, huna biashara, unawasindikiza tu wengine. Kama siku usipofungua biashara wateja hawakwami kwenye mahitaji yao, wateja ulionao ni kwa hisani tu, siyo wako.

Lazima uwe na kitu cha kuitofautisha biashara yako na wengine wanaofanya biashara kama yako. Kitu ambacho wengine hawawezi kukiiga kabisa.

Utaweza kuwa na kitu hiki kama wazo lako la biashara umelitengeneza mwenyewe na siyo kuiga wengine. Pia kwa kuwa na mfumo mzuri wa biashara, unaiwezesha kuwa na ufanisi mzuri kwenye kila eneo kitu kinachowafanya

wateja wapende kuja kwako kwa sababu wanapata huduma nzuri.

Wakati mwingine unahitaji kuwa na siri fulani au hatimiliki ya yale unayofanya kwenye biashara ili kuhakikisha hakuna anayeweza kukuiga na kukuondoa kwenye biashara yako.

Kadiri biashara inavyokuwa ya kipekee na kutegemewa na wateja wake ndivyo inavyokuwa huru.

## Kudumu.

Kitu cha tatu muhimu kufikia uhuru wa kibiashara ni kudumu, lazima uwe na mkakati wa kuiwezesha biashara yako kudumu kwa miaka mingi.

Usifanye biashara kwa kuangalia faida ya leo tu, angalia faida ya miaka 10, 20 mpaka 50 ijayo. Watu wengi wamekuwa wanakimbiza faida za muda mfupi na zinaishia kuwa kikwazo kwao kupata faida za muda mrefu.

Kuwa na mfumo wa kuiendesha biashara na kitu kinachoitofautisha ni hatua muhimu za kuiwezesha kudumu.

Hatua nyingine ni kufanya uwekezaji endelevu kwenye biashara yako. Kwa kila faida unayoipata, sehemu rudisha kwenye biashara ili kuiwezesha ikue zaidi. Pia tumia fursa mbalimbali za kuendelea kukuza mtaji wa biashara yako na kutoa huduma bora zaidi kwa wateja.

Hatua nyingine muhimu ya kuiwezesha biashara kudumu ni kuhakikisha inaweza kujiendesha hata kama haizalishi faida. Kama tulivyoona kwenye fedha binafsi, kwenye biashara pia unapaswa kuwa na akiba ya kuiwezesha biashara kuiendesha kwa kipindi cha miezi sita mpaka mwaka hata kama haizalishi faida kabisa.

Biashara nyingi haziwezi kujiendesha hata kwa mwezi mmoja kama hazina faida, kitu kinachosababisha nyingi kufa hasa pale zinapopitia misukosuko mbalimbali. Wewe

ijengee biashara yako akiba ya kuweza kujiendesha kwa angalau miezi sita mpaka mwaka hata kama haizalishi faida kabisa.

Kwa biashara yako kuwa na akiba hiyo, inakuwa huru kukabiliana na chochote bila ya kufa. Hata kama ni ushindani mpya umejitokeza, biashara inakuwa na uwezo wa kuhimili wakati unaendelea kutafuta njia za kukabiliana na ushindani huo.

Jambo jingine muhimu kwenye kujenga uhuru wa kibiashara ni biashara kutokutegemea mteja mmoja mkubwa au wachache. Biashara inapaswa kuwa na wateja wengi kiasi kwamba wachache wakikwama au kuondoka biashara haitetereki haraka.

Zingatia haya katika kujenga biashara inayokuwa huru na kukupa wewe uhuru mkubwa.

# UHURU WA MAISHA.

Uhuru wa mwisho tunaokwenda kujifunza kwenye barua hii ni wa kuyaishi maisha yako kwa namna ambayo ni sahihi kwako.

Unaweza kuwa na uhuru binafsi, uhuru wa fedha na aina nyingine za uhuru tulizojifunza, lakini maisha yakakunyima uhuru, ukajikuta unaendesha maisha ambayo huna uhuru kabisa.

Kwenye maisha kwa ujumla, kuna mifumo mitatu ambayo inapambana kukunyang'anya uhuru wako. Unapaswa kuijua mifumo hii na jinsi inavyofanya kazi ili kuhakikisha haiondoi uhuru wako.

## Jamii.

Jamii huwa hazipendi watu ambao ni huru na wanaoishi vile wanavyotaka wao. Badala yake huwa inapenda watu ambao wanaishi kama jamii inavyowataka waishi. Lakini ukiishi kama jamii inavyotaka uishi huwezi kuwa huru, kwa sababu jamii haijui unachotaka au unachothamini.

Hivyo ni muhimu uwe tayari kutofautiana na jamii kwenye baadhi ya mambo ili uwe na maisha huru.

Kwanza kabisa jua taratibu mbalimbali zilizopo kwenye jamii na kisha hoji kila utaratibu na usahihi wake. Taratibu nyingi zimepokelewa kwa mazoea na hazina maana yoyote, lakini zimewafunga wengi. Hivyo kuwa mtu wa kuhoji na kujua ukweli badala ya kukubaliana na kila kitu.

Mbili usiwe mtu wa kufuata mkumbo, kwa sababu kila mtu anafanya kitu haimaanishi na wewe ni lazima ufanye. Ndani yetu tuna mazoea ya kufuata mkumbo, kuona kinachofanywa na wengi ndiyo sahihi. Lakini huo siyo ukweli, mara nyingi kinachokubalika na wengi ni kile ambacho siyo kigumu na vitu vingi ambavyo siyo vigumu huwa siyo sahihi.

Tatu usianzishe migogoro ambayo haina manufaa yoyote. Usitake kuona wewe ndiyo bora au unayeuona ukweli zaidi ya wengine. Chagua kuyaishi maisha yako na waache

wengine waishi maisha yako. Usilazimishe kila mtu akubaliane na wewe au aishi kama unavyoishi wewe. Pia usitumie muda mwingi kutetea maisha uliyochagua kuyaishi. Wewe ishi maisha yako, kwa kufanya kilicho sahihi na walio sahihi watakuelewa bila hata kupiga kelele, huku wasio sahihi kutokuuelewa hata uwaambie nini.

Kazana kujenga mahusiano mazuri na imara kwako, kwa wale ambao mnaweza kwenda pamoja na usitake kukubaliana au kuendana na kila mtu.

## Dini.

Dini zimekuwa chanzo cha wengi kukosa uhuru kwenye maisha yao. Dini zimekuwa na sheria nyingi ambazo hazina maana yoyote. Sheria hizi ukiziangalia kwa undani, unaona hazina mchango wowote katika kumsaidia mtu kukua kiroho, bali lengo lake ni kumfanya muumini awe mtumwa kwa dini husika.

Hivyo kwa dini yoyote unayochagua kuwa ndani yake, linda uhuru wako binafsi. Linda nafasi ya

wewe kuhoji kila kitu na kuthibitisha mwenyewe badala ya kulazimishwa kuamini kila kitu kama unavyoambiwa.

Lengo lako kubwa linapaswa kukua kiroho na hivyo kama dini uliyonayo haikusaidii kwenye hilo, siyo sahihi kwako.

Kama dini inatumia vitisho kwako kukufanya ujawe na hofu na kupokea yale unayoambiwa siyo sahihi, inakunyima wewe uhuru.

Dini inapaswa kukuwezesha kujitambua, kuishi maisha ya kusudi lako, kuwa na upendo na kufanya yaliyo sahihi kwako na kwa wengine.

Kama dini inakusisitiza kwenye mambo mengine tofauti na hayo, inakupoteza. Kama kila wakati unaambiwa kuhusu kuondolewa mapepo, kukingwa na wachawi na kuwa tegemezi kwa viongozi wa dini katika kutatua changamoto za maisha yako unageuzwa kuwa mtumwa.

Njia nzuri ya kujienga kiroho kama dini yako haikusaidii hilo ni kuchagua kuishi kama

alivyoishi yule ambaye dini imeasisiwa kupitia yeye. Mfano kwenye Ukristo, chagua kuishi kama Yesu, kwenye Uislamu chagua kuishi kama Muhamad, kwenye Uhindu ishi kama Krisha, Ubudha ishi kama Budha. Na kama huna dini, chagua falsafa unayoikubali na inayoendana na wewe kisha chagua mwanafalsafa utakayeishi kama yeye.

Dini zimegeuza wengi kuwa watumwa, kwa kuwazuia kuwa huru, kujifunza na kuhoji mambo mbalimbali. Dini zimekuwa na nguvu kubwa ya kuwashikilia wengi kwenye utumwa kwa sababu watu wamekuwa wanapandikizwa tangu wakiwa watoto.

Usiogope kuchukua uhuru wako kutoka kwenye dini inayokukandamiza. Fanya hivyo kimya kimya, usipambane na yeyote, usibishane na yeyote na wala usione wewe ni bora au unajua kuliko wengine. Jua lengo lako ni kufikia ukuaji wa kiroho, chagua jinsi utakavyoyaishi maisha yako kwa msingi sahihi na yaishi hivyo.

## Serikali.

Serikali yoyote ile duniani, huwa haipendi watu walio huru, hakuna atakayekuja kukuambia hili, lakini hivyo ndivyo ilivyo. Wananchi walio huru na wanaojielewa ni vigumu kuongozwa na serikali kwa sababu serikali kama taasisi kubwa inaendeshwa kwa urasimu, hivyo vitu vingi huwa havifanywi kwa usahihi.

Ili kuhakikisha inalinda nguvu yake, serikali imekuwa inatunga sheria nyingi na ambazo zinaweza kuwa hata zinakinzana lakini hazitumiki wazi wazi. Lengo ni siku ikitaka kumtia mtu yeyote hatiani, isikose sheria ya kufanya hivyo.

Mtu yeyote yule kwenye nchi yoyote na kwa wakati wowote, kuna sheria anavunja, ila hasumbuliwi kwa sababu serikali haina tatizo naye. Lakini ikatokea siku serikali ina tatizo na mtu, ikianza kumulika maisha yake, kuna sheria nyingi atakazokuwa anazivunja na hivyo hakitakosekana kitu cha kumtia hatiani.

Kwa kujua hili, unapaswa kuwa na njia ya kulinda uhuru wako dhidi ya serikali. Kuna hatua tatu muhimu za kuchukua katika kukamilisha hilo.

Moja ni kufuata sheria na taratibu zote kadiri ya uwezo wako. Jitahidi mno kufuata kila sheria na taratibu unayoijua na kadiri unavyoweza. Japo hutaweza kufuata zote kwa sababu nyingi zinakinzana na kuna nyingine huzijui, lakini hakikisha kwa kadiri ya uwezo wako unafuata sheria na taratibu za nchi.

Mbili ni kujihusisha na serikali kwa kiwango cha chini kabisa. Timiza wajibu wako kama mwananchi kwa kufuata sheria, kulipa kodi na kusaidia wengine kwa kadiri unavyoweza. Lakini zaidi ya hapo, punguza kujihusisha na serikali, hasa kwenye biashara. Kama nilivyokueleza hapo juu, serikali duniani kote huwa zinaendeshwa kwa urasimu, hivyo hakuna mtu mmoja ambaye anaweza kuumizwa na kosa analofanya, ni mfumo. Sasa unapojihusisha nayo kama mtu binafsi, utajikuta unaumia wewe zaidi. Mfano kama unaiuzia serikali

bidhaa au huduma fulani, unaweza kuwa una madai yako unapaswa kulipa, lakini yakachukua muda mrefu na hakuna anayejali, wewe biashara yako inaumia kwa kukosa fedha, huku wanaopaswa kuchakata malipo yako wakiwa hawaumii na hivyo hawaharakishi kukamilisha malipo yako.

Tatu ni tengeneza uwezo na siyo kutafuta upendeleo. Njia ambayo wengi wamekuwa wanapoteza uhuru wao ni kutafuta upendeleo kutoka kwa wale walio serikalini. Hivyo wanapewa nafasi kwa sababu wamejipendekeza na siyo kwa sababu ya uwezo. Yeyote anayekupa nafasi kwa upendeleo, atakugeuza kuwa mtumwa kwake. Lakini unapokuwa umeipata nafasi kwa uwezo wako binafsi, unakuwa huru.

Kazi na biashara unazofanya, zijengee uwezo wa kusimama zenyewe na siyo kutegemea upendeleo wa wale walio kwenye nafasi za madaraka. Maana hawa huja na kupita, lakini mafanikio unayojenga na uhuru unaotaka ni wa kudumu kwa muda mrefu.

Kingine muhimu kwenye kujenga uhuru wako kutoka kwenye serikali ni kujihadhari na wanasiasa. Hawa huwa wanapenda kutumia kila namna kukamilisha mahitaji yao na wakishapata wanachotaka, hawajali tena. Epuka kutumiwa na wanasiasa kukamilisha matakwa yao.

Uhuru wa kimaisha unakutaka ujue jinsi jamii, dini na serikali vinavyojiendesha ili kuwafanya watu wawe tegemezi kwenye mifumo hiyo, kisha wewe uchague kuyaishi maisha yako kwa namna ambayo utapunguza mikwaruzano na mifumo hiyo.

## HITIMISHO.

Kwenye barua hii tumejifunza kuhusu uhuru kamili na jinsi a kuufikia. Umejifunza mengi hapa, na mengi siyo rahisi, hivyo ni mchakato ambao ni endelevu. Muhimu ni kwa kila hatua unayochukua kwenye maisha yako kujua mapema kama inakujengea uhuru zaidi baadaye au inakuwa kikwazo kwa uhuru wako.

Mara zote chukua hatua ambazo zinakujengea uhuru zaidi na epuka sana hatua zinazokuwa kikwazo kwa uhuru wako wa sasa na wa baadaye.

## MAONI, SHUHUDA NA MASWALI.

Karibu kwa maoni, shuhuda na maswali kuhusu barua hii.

Kama kuna mahali hujaelewa na ungependa ufafanuzi zaidi basi karibu uulize swali.

Kama kuna eneo unaweza kuongeza maoni zaidi karibu pia.

Na kama una ushuhuda wa namna umewahi kufanyia kazi yale uliyojifunza kwenye barua hii, karibu utushirikishe matokeo ambayo uliyapata.

Maoni, maswali na shuhuda viwekwe moja kwa moja kwenye kundi la KISIMA CHA MAARIFA wasap.

Nikutakie kila la kheri katika kufanyia kazi haya uliyojifunza kwenye barua hii.

Rafiki yako anayekupenda sana,

Kocha Dr. Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com/kocha

0755 953 887 / kochamakirita@gmail.com

**MUHIMU;** KAMA HUJAPATA BARUA ZA NYUMA, FUNGUA; www.kisimachamaarifa.co.tz/barua2021